

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI



Simu Na: +255 (027) 29 - 77402
Nukushi: +255 (027) 29 - 77402
Barua Pepe: ded@handenidc.go.tz
Tovuti: <http://www.handenidc.go.tz>

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Handeni,
S. L. P 355,
HANDENI.
18/11/2021

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni anawatangazia wananchi wote nafasi za Kazi ya Mtendaji *wa Kijiji III* kama ifuatavyo;

a) **Idadi ya Nafasi (Nafasi 03)**

b) **Majukumu ya Mtendaji wa Kijiji Daraja la III**

- i. Kuwa Katibu wa Mikutano na kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- ii. Atakuwa Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- iii. Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala Bora katika kijiji.
- iv. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango wa Maendeleo ya Kijiji.
- v. Kuwa Mshauri wa Serikali ya Kijiji kuhusu Mipango ya Maendeleo katika Kijiji.
- vi. Msimamizi wa Utekelezaji wa Sheria Ndogo pamoja na Sheria nyingine zinazotumika katika Kijiji.
- vii. Atakuwa Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalam waliopo katika kijiji.
- viii. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
- ix. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata ambayo kijiji chake kipo.
- x. Kiongozi wa wakuu wa Vitengo vya kitaalamu katika kijiji.
- xi. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- xii. Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.

c) **Sifa za Mwombaji**

- i. Awe raia wa Tanzania
- ii. Awe amehitimu na kufaulu Elimu ya Kidato cha IV na zaidi na vyeti vyake viwe halali visivyo na shaka yoyote.
- iii. Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo: **Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa** kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo-Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.
- iv. Awe na Umri wa kuanzia miaka 18 hadi 45.
- v. Testimonials, Provisional results, statement of results na hati za matokeo ya kidato cha IV na VI (result slips) HAVITARUHUSIWA
- vi. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimethibitishwa na Mamlaka husika (NECTA au NACTE)
- vii. Maombi yaandikwe kwa mkono na mwombaji kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza.

d) **Aina ya Ajira na Mshahara;**

- i. Ajira hii ni ya Masharti ya KUDUMU (Permanent & Pensionable) na Mshahara wake utakuwa katika ngazi ya TGS B.1

e) **Nyaraka/Taarifa za Kuambatisha kwenye Maombi**

- i. Taarifa binafsi inayojitosheleza (C.V)
- ii. Nakala za Vyeti vya Elimu na Mafunzo
- iii. Cheti cha kuzaliwa
- iv. Mawasiliano - hususani namba za simu (*Mobile Number*)
- v. Picha 2 za rangi (*Passport Size*)


f) Muda wa Kutuma Maombi ni kuanzia tarehe **22 Novemba hadi tarehe 05 Desemba, 2021** Saa 9.30 Alasiri. Baada ya hapo Maombi hayatapokelewa.

Maombi yote yatumwe kupitia anuani ifuatayo;

*Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya
S.L.P 355*

HANDENI

Limetolewa na:-



Saitoti Z. Stephen

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HANDENI**